

**MAKUBALIANO YA KUANZISHA UHUSIANO WA KIRAFIKI KATI YA WILAYA
YA TARIME (TANZANIA) NA JIJI LA MILWAUKEE (AMERICA)**

Ambapo, Programu ya Uhusiano wa kirafiki wa Jiji, inayosimamiwa na Uhusiano wa Kimataifa wa Urafiki wa Majiji, ilianzishwa na Rais wa Amerika mwaka 1956 kuhimiza urafiki mkubwa na maelewano kati ya Amerika na mataifa mengine kwa njia ya mawasiliano ya binafsi ya moja kwa moja; na


Ambapo, Ili kuimarisha malengo yale, watu wa Jiji la Milwaukee na Wilaya ya Tarime kwa ishara ya urafiki na nia njema, wanakubali kushirikiana kwa lengo la faida ya pamoja ya jumuiya zao kwa kupata fursa za kielimu, kiuchumi na kiutamaduni; na

Ambapo, Tunakubali kuunga mkono na kuhimiza fursa kwa ajili ya ubadilishajanaji wa faida halisi za pamoja zitokanazo na masuala ya biashara, utamaduni, huduma za afya, elimu na utalii; na

Ambapo, Jiji la Milwaukee na Wilaya ya Tarime, zina mtizamano sawa wa elimu, huduma za afya na biashara, na shauku ya kuinua maelewano mazuri ya pamoja miongoni mwa raia wetu kwa kutangaza wenyewe kuanzishwa kwa Uhusiano wa Majiji tarehe Julai 6, 2016, tarehe ambayo Halmashauri ya Milwaukee ilipitisha uamuzi wa kuanzisha Uhusiano wa Kirafiki Jiji.

Kwa hiyo basi sasa, Jiji la Milwaukee na Wilaya ya Tarime zinatanganza wenyewe Uhusiano wa Majiji, na kutamka nia yao ya kuzingatia miongozo hii kulingana na Sera za Kimataifa za Uhusiano wa Majiji.

Imesainiwa Novemba 7, 2016 kwa nakala mbili za lugha ya Kiswahii na Kiingereza, nakala zote mbili zina maana sawa.



Mhe. Moses Matiko Misiwa
Meya wa Wilaya ya Tarime



Ashanti Hamilton
Rais wa Baraza la Mji wa
Milwaukee